



(Shikamaneni na) Swala nyinyi na waliomilikiwa na mikono yenu ya kuume

Imepokelewa kutoka kwa Anas radhi za Mwenyezi Mungu ziwe ju yake amesema: Ulikuwa usia mkubwa wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake alipofikwa na mauti:

"(Shikamaneni na) Swala nyinyi na waliomilikiwa na mikono yenu ya kuume,

(Shikamaneni na) Swala nyinyi na waliomilikiwa na mikono yenu ya kuume", mpaka akaanza Mtume rehema na amani ziwe juu yake kushikwa na kwikwi kifuani kwake kwa maneno hayo kwa sababu ya kifo, na maneno hayo yalikaribia kujaa ulimi wake.

[Sahihi]

Ulikuwa usia mwingi wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake kwa Umma wake naye akiwa katika ulevi wa kifo: Shikamaneni na swala na mdumu nayo na wala msighaflike nayo, na vile vile timizeni haki za wale wanaomilikiwa na mikono yenu ya kuume miongoni mwa watumwa na wajakazi na wamilikini kwa wema, akaendelea kuukariri, mpaka ukaanza kumkwama katika koo lake, na ulimi wake ukashindwa kuutamka kwa ufasha.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/66359>